

Fikiria ili Ufanikiwe

*Jifunze Jinsi ya Kufikia Malengo Yako
Kutatua Matatizo na Kufanya Mambo*



NDIYO!
Ninaweza!

**Zana ya Kusaidia
Kufikiria
Imejumuishwa**

*Pakua Kitabu cha
Bila Malipo*

EducationalMissions.org



Ni wajibu wako!


*Unapobadilika, kila kitu
kinabadilika.*

Rafiki yangu, hatimaye ni zamu yako kugundua kanuni ambazo zimesaidia mamilioni ya watu kufanikiwa katika kila sehemu ya maisha yao. Ukizitumia kwa makini, kanuni hizi zitakusaidia kutatua matatizo, kuleta matumaini, furaha, na bila shaka ufanisi katika matumizi ya fedha. Familia mbalimbali zimeinuliwa kutoka katika umaskini mkubwa, matumaini yamerejeshwa, na himaya kubwa za kifedha zimejengwa. Sasa, vyote hivi ni vyako kuvipata!

Unaweza kuchukua jukumu la maisha yako leo.

Je, uko tayari kwa ajili ya mabadiliko? Je, uko tayari kufanya jambo linalohitaji kufanywa? Ili kufanikiwa, unahitaji juhudi, muda na nguvu. **Habari njema!** Tutakusaidia kufanya kazi kwa akili zaidi, sio kwa kutumia nguvu zaidi. Mfumo huu wa hatua kwa hatua. Utakaojifunza utakusaidia kuwa mwenye mipangilio zaidi, mwenye matokeo zaidi na kukufundisha jinsi ya kutatua matatizo ambayo yanakuzuia.

Wewe ndiye mtu pekee ulimwenguni unayeweza kutimiza maono, malengo na ndoto zako. Unaweza kutimiza chochote unachotaka kutimiza maishani - ikiwa utakuwa tayari kujituma. Unaweza kupanga mustakabali wa maisha yako ya mbele! Hayo ni maisha yako; yaishi kikamili. Usiridhike na kidogo. **Unastahili kilicho bora zaidi!**



EINSTEIN THINKERS

na **Educational Missions** wanayo furaha kukuletea zana ya utambuzi ya kusaidia kukumbuka ya **LOGICDIE™**. Utambuzi unatokana na uwezo wa kufikiria, huku zana za kusaidia kukumbuka zitakusaidia kuboresha kumbukumbu.

Kamusi ya Lugha ya Oxford inafafanua utambuzi (cognition) kuwa, *“tendo la kiakili au*

mchakato wa kupata maarifa na ufahamu kupitia mawazo, uzoefu na hisia. ”

Mafanikio yako yatakuwa yameunganishwa moja kwa moja na uwezo wako wa kupata maarifa na ufahamu wa kile unachotaka na jinsi ya kukipata! Einstein alifundisha, *“Hatuwezi kutatua matatizo yetu kwa kutumia mawazo yaleyale tuliyotumia kuyasababisha.”* Kama Einstein yuko sahihi, basi tunahitaji kubadilisha namna yetu ya kufikiri.

LogicDie ni mfumo rahisi kuukumbuka wa hatua kwa hatua kwa ajili ya kutatua matatizo na kufikia malengo yako. Kila upande unawakilisha kanuni ya biashara kwa ajili ya kupata maarifa na kuendeleza mpango wa vitendo. Kanuni hizo zitakusaidia kujipatia pesa na kuwa na hali nzuri kifedha . Muhimu zaidi, utazitumia katika kila nyanja ya maisha yako. Unaweza kuzitumia kujenga mahusiano thabiti, kutatua matatizo au hata kubadilisha ulimwengu.

Fikiria ili Ufanikiwe

Geuza Ndoto za Leo kuwa Maisha Halisi ya Kesho!

Tatua Matatizo - Punguza Mfadhaiko - Timiza Mambo!

**Jifunze jinsi ya kuunda mipango ya mafanikio
katika kila nyanja ya maisha yako!**

*Fuata hatua hizi rahisi ili kutengeneza mpango mkakati ili
kutimiza malengo yako, kukamilisha miradi na kutatua matatizo.*



Jitahidi Kadri Uwezavyo - Anza na mtazamo unaofaa. Jitolee mwenyewe - kufanya kadri uwezavyo. Unastahili kile kilicho bora zaidi kutoka kwako. Mama zetu walitufundisha kufanya kila tuwezavyo kila wakati.

Zingatia - Jambo Moja kwa Wakati

Kuzingatia kunajumuisha kufafanua lengo lako na kulifanyia kazi. Lazima ujue unachotaka na upange jinsi ya kukifikia . Kuzingatia kunahitaji fikra wazi juu ya mahali ulipo sasa na mahali unapotaka kuwa. **Akili yako hukumbuka mambo katika picha.** Tengeneza taswira au picha kichwani ukifikia malengo yako. Yaone kwa macho ya akili yako. Andika kumbukumbu za mawazo yako. Kumbukumbu hizi za maandishi hukupa uwazi na kukupa ramani ya kufuata. Kuzingatia kwako huathiri mipango yako na mchakato wa kufanya maamuzi.



Epande 1



Upande 2

Gawanya ili Kufanya Maamuzi –

Rahisisha miradi na maamuzi yako kwa kuivunja katika sehemu ndogo zinazoweza kushughulikiwa; gawanya ile ufanye maamuzi. Kwa namna gani? Kwa kujiuliza maswali mazuri. Nini, wapi, kwa nini, lini, nani, na jinsi gani? Majibu ya maswali hayo yatakusaidia kuelewa vizuri zaidi na kukuongoza. Anza kwa kutengeneza orodha; ni mambo gani unayajua na usioyajua? Zingatia faida na Hasara. Kuwa na mtazamo chanya. Kuna zaidi ya njia moja ya kukamilisha jambo. Tafuta njia mpya na mitazamo mipya.

Tafuta Ushauri wa Hekima – Tafuta majibu!

Tafuta ushauri kutoka kwa wataalamu waliofanikiwa katika kile unachotaka kufanya. Soma vitabu vyao. Fanya utafiti wako mwenyewe! Nenda kwenye maktaba. Tafuta katika intaneti. Tumia Google, Bing au YouTube. Zungumza na wazee. Usiridhike na jibu la kwanza unalopata. Kuna uwezekano mkubwa wa kufanikiwa ikiwa utapata maoni kutoka kwa washauri wengi. **Andika ushauri wao!**



Upande 3




Karatasi na Penseli -

Kuandika huchangia sana katika mafanikio yako kwa ujumla. Kunakupa uwezo wa kupangilia mtazamo na mawazo yako. Mpango mzuri siku zote unaanza na maelezo yaliyoandikwa. Ukichunguza utagundua kwamba kila kitu kilichovumbuliwa na mwanadamu, isipokuwa vichache, kilianza na wazo. Mtu fulani aliandika mawazo yake; kisha

akajitahidi kutengeneza mpango. Andika mtazamo na mawazo yako ili uweze kuyapangilia. Kumbukumbu za maandishi hazipitwi na wakati; zinakuwezesha kuanza na kukamilisha miradi mingi ya maisha yako. Kumbukumbu zako za maandishi zitakusaidia kuendeleza miradi yako mbele.

Panga - Panga kumbukumbu zako za maandishi katika sehemu **nne**. Hii itakusaidia kuweka vipaumbele, pamoja na kurahisisha mambo. Sasa tengeneza **Orodha yako ya Mambo ya Kufanya**. Orodha hii itaweka miongozo ya kile unachohitaji kufanya baadaye na kuboresha ufanisi wako. Ufanisi wako utaathiri moja kwa moja mafanikio yako kwa ujumla.



1.) **Sehemu ya Kutupwa**. Ondoa mawazo mabaya na mawazo. Hata hivyo, mawazo makubwa sio mabaya kila siku. Sehemu hii ni kama pipa la taka.

2.) **Sehemu ya Mambo Yanayoweza Kufanyika**. Sehemu hili inajumuisha majukumu ambayo unajua yanaweza kutekelezeka. Una kila kitu unachohitaji ili kukamilisha mambo yaliyopo kwenye sehemu hii. Hakuna kitu kinachokuzuia bali ni wewe mwenyewe. Hakuna kisingizio kwa kutokamilisha mambo haya.

3.) **Sehemu la Mambo Yanayowezekana**. Hii inajumuisha mambo unayojua unaweza kutimiza, lakini kuna kitu kinachokosekana ambacho kinakuzuia. Mambo yanawezekana, "ikiwa" ungekuwa na hiki... au "ikiwa" ungekuwa na kile...

Kitu unachokosa ndicho pekee kinachokuzuia. Vizingiti hivi vinaweza kuwa kwa mfano kukosa muda, pesa, rasilimali au hata msaada. Lazima utambue kwa uwazi vizingiti hivi vya “ikiwa.” Kusuluhisha vizingiti hivi vya “ikiwa” ndio ufunguo wako wa mafanikio. Ili kubadilisha mambo haya kuwa mambo yanayofanyika, fuata ushauri uliopata kutoka kwa wataalamu. Ongeza majukumu kwenye orodha yako ya mambo ya kufanya. Fanya kile kinachohitajika kufanywa. Ikiwa bado una changamoto, endelea kutafuta ushauri kwa watu wenye hekima. Kuna mtu fulani utampata ambaye atakuwa na majibu unayohitaji. Endelea kuongeza bidii. Utapata suluhisho usipokata tamaa. Tunashindwa pale tu tunapokata tamaa. Jiamini; endelea kutafuta suluhu ambayo ni sahihi. Unaweza kufanya jambo lolote!

Maelekezo ya jinsi ya kuondoa kizingiti hicho cha “ikiwa” ambacho kinakuzuia.

- a. **Fanya Kadri Uwezavyo** - Jitoe kikamilifu.
- b. **Zingatia** - Fafanua kwa uwazi shabaha au lengo lako.
- c. **Gawanya ili Uamue** - Jiulize maswali yanayofaa.
- d. **Tafuta Ushauri wa Hekima** - Tafuta majibu kutoka kwa wataalamu.
- e. **Andika Mawazo Yako** - Yapange na uchukue hatua.

Rudia hatua hizi mara nyingi inavyohitajika ili kufanikiwa.

4.) ***Sehemu ya Ndoto.*** Sehemu hii ni ya mawazo makubwa ambayo yatahitaji muda na kufikiria ziada. Inapendekezwa uanze kwa kutengeneza orodha yako ya mambo ya kufanya. Ingawa, ndoto kubwa zina vikwazo vingi vya “ikiwa”, usiruhusu vikwazo hivyo vikuzuie. Usikate tamaa. Tambua vikwazo vya “ikiwa” ambavyo vinakuzuia. Viondoe moja baada ya kingine hadi ndoto yako itimie.



Pima Maendeleo Yako - Orodha ya Mambo ya Kufanya!

Kuchukua hatua ndiyo njia pekee ya kusonga mbele. Miradi au kazi hukamilishwa kwa kuchukua hatua moja baada ya nyingine. Tambua wazi kazi inayohitaji kukamilishwa na uiongeze kwenye orodha yako ya mambo ya kufanya. Katika mchakato wa kupanga utaweza kubaini idadi ya kazi zinazohitajika kukamilishwa ili kufikia lengo lako kwa mafanikio. Upane wa tano wa **LOGICDIE** hukusaidia kupima maendeleo yako. Kila wakati unapokamilisha shughuli huwa umesogeza gurudumu lako hatua moja karibu na lengo lako. Habari njema ni kwamba miradi mingi inahitaji tu hatua 5, 6 au hata chini yake ili kukamilika kwa ufanisi. Hatua ndio njia PEKEE ya kupata matokeo. Ni sawa kufanya kidogo kidogo kwa wakati mmoja. Ni kawaida. Kusonga mbele kwa uthabiti kutahakikisha unafikia malengo yako. **Ninakuamini WEWE!**



**Simon kutoka kijiji cha
OTICI nchini Uganda ni
mmoja wa mashujaa wangu!**

Alipokuwa mtoto, alitoroka
vita **vya**
kaskazini vilivyokuwa
vikipiganwa kaskazini na
akalelewa katika kituo cha

watoto yatima. Amejitahidi kila siku na kuazimia kutoruhusu hali yake duni imzuie kufikia lengo lake, na wewe pia hupaswi kuruhusu hali yako ikuzuie.

Alikuwa mwanafunzi katika Shule ya ~~Upili~~ ya ~~Yale~~ Sekondari ya Yale huko Kayunga alipofanya uamuzi mkubwa maishani. Ulikuwa uamuzi wa kujifunza na kutumia kanuni za **LOGICDIE**. Alianza kwa kuwafundisha marafiki na wanafunzi wenzake mfumo huu wa hatua kwa hatua wa kufikia malengo. Tangu wakati huo, Simon ametimiza mambo makubwa. Amejenga kituo cha jamii, amefungua shule inayowasaidia mamia ya watu na kuishawishi serikali kujenga barabara ya kuelekea kijijini kwao. Ameanzisha biashara mbalimbali, kwa mfano saluni na ukumbi wa maonyesho. Alianza kilimo na analima mimea na kufuga mifugo. Ametengeneza ajira kwa jamii yake na kwingineko.

Simon ametumia kwa busara kanuni za **LOGICDIE™** ili kutimiza malengo na ndoto zake. **Na unaweza kufanya hivyo pia!**